

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Simu: +255-26-2323189

Barua pepe: ps@moha.go.tz

Tovuti: www.moha.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,

Mtaa wa Habari/Afya,

S.L.P. 2916,

40483 DODOMA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WAJIBU WA VIONGOZI WA DINI**  
**KUELEKEA UCHAGUZI MKUU OKTOBA 28, 2020**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayo wajibu wa kusajili na kusimamia jumuiya za kijamii na taasisi za dini. Jumuiya hizo husajiliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya Sura ya 337 kama ilivyofanyiwa Marekebisho na Sheria Namba. 3 ya Mwaka 2019.

Hivi karibuni kumeibuka tabia ya baadhi ya viongozi wa kidini na wanaojiita viongozi wa dini ambao wanatumia nyumba za ibada na majukwaa ya kisiasa kueleza kuwa taasisi zao au makundi yao yanamuunga mkono au wanamuunga mkono mgombea fulani, na wakimuahidi kumpigia kura mgombea huyo.

Aidha, Viongozi wengine wameonekana wakihamasisha na kutoa maelekezo kwa waumini wao kumchagua mgombea fulani. Vitendo hivyo ni kinyume na kifungu cha 17 (c) cha Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Namba 3 ya Mwaka 2019 na Kanuni zake.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inawakumbusha viongozi wote wa taasisi za dini na Jumuiya za Kijamii kuepuka kutoa matamko ya kisiasa yenye lengo la kuhamasisha au yenye viashiria vya kuhamasisha na kuelekeza waumini wao kuchagua mgombea au chama fulani, **badala yake wazingatie Sheria ya Jumuiya ambayo inakataza viongozi wa kidini kujihusisha na vitendo hivyo, kwa kuwa vinaingilia uhuru wa kikatiba wa kila mtu kumchagua mgombea anayemtaka.**

Wizara inatoa wito kwa taasisi zote za dini na Viongozi wote wa dini nchini, kuacha kutumia majukwaa ya kisiasa na nyumba za ibada kuhamasisha na kuchochea waumini kuchagua au kutokuchagua mgombea au chama fulani badala yake wajikite kwenye kuhubiri amani, upendo na umoja. Viongozi watakaoshindwa kuzingatia masharti ya Sheria za Usajili wa Jumuiya na Katiba zao, Wizara haitasita kuchukua hatua za kuifuta Jumuiya hiyo au kutoisajili ambayo imewasilisha maombi yake.

Imetolewa leo tarehe 20 Oktoba, 2020 na:

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'George Boniface Simbachawene'.

George Boniface Simbachawene  
**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**